

Kutoa Hati ya Mapato Yako

Ili kutuma ombi la UNM Care au Out-of-County Care, lazima utupatie hati za kuthibitisha ajira na mapato yako. Njia moja ya kufanya hili ni kutupatia nyaraka za mshahara. Hapa kuna njia nyingine mbili za kutoa hati ya mapato yako ikiwa huwezi kutoa nyaraka za mshahara.

- Unaweza kumwomba mwajiri wako atoe taarifa iliyoandikwa (barua ya uthibitisho wa ajira) inayothibitisha ajira na mapato yako (ukurasa wa 2).
- Unaweza kutoa taarifa ya mapato yako ukitumia Fomu ya Mapato iliyoambatishwa (ukurasa wa 3).

Kwa barua ya uthibitisho wa ajira unaweza kumpatia mwajiri wako maelekezo yaliyo hapa chini.

Mpendwa Mwandishi wa Barua,

Asante kwa kuniandalia taarifa. Hapa kuna baadhi ya maelekezo

- **Unaweza kutumia Barua ya Uthibitisho wa Ajira ya mfano** iliyo katika ukurasa unaofuata. Nakili barua hiyo ya mfano na uibandike kwenye ukurasa ulio na lebo ya shirika lako (ikiwa unayo), ujaze nafasi tupu na utie sahihi.
- **Unaweza kuandika Barua ya Uthibitisho wa Ajira kwa mkono.** Tumia barua ya mfano iliyo katika ukurasa unaofuata kama mwongozo kuandika barua yako mwenyewe. Kwa barua zilizoandikwa kwa mkono au barua zisizo na lebo, pia jumuishia kadi rasmi ya maelezo ya mawasiliano ya biashara au hati kama hiyo.
- Barua zote lazima ziwe na tarehe, jina la mwandishi, cheo, nambari ya simu na barua pepe ya mawasiliano na sahihi.
- Barua zinaweza kupeanwa kwa mgonjwa moja kwa moja ili aziwasilishe mwenyewe au zinaweza kutumwa kwa barua ya posta kwa UNM Financial Assistance katika 1131 University Blvd, Suite D, Albuquerque, NM 87102 au zinaweza kutumwa kwa barua pepe kwa financialassistance@salud.unm.edu au anwani ya barua pepe ya mwakilishi wa mgonjwa.
- Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali pigia simu kitengo cha Usaidizi wa Kifedha cha UNM kwa 505 272-2521.

Barua ya Uthibitisho wa Ajira ya Mfano

Tarehe: _____

Tafadhali kubali barua hii kama uthibitisho wa kuajiriwa kwa _____
jina la mfanyakazi

sasa hivi katika _____
jina la kampuni

_____ amefanya kazi nasi tangu _____
jina la mfanyakazi mwezi/mwaka

Analipwa kiasi cha \$ _____ kwa kila (*chora duara katika chaguo moja*) siku, wiki, wiki mbili, mwezi.

Ikiwa una maswali yoyote au unahitaji maelezo yoyote ya ziada, tafadhali jisikie huru kuwasiliana nami kwa _____.

Sahihi

Jina

Cheo

Jina la kampuni

Nambari ya simu na/au anwani ya barua pepe

Fomu ya Mapato (Mapato ya Wastani ya Miezi 6)

1. Fedha Zilizochumwa

Pesa zilizochumwa	Mfano	Mwezi wa 1	Mwezi wa 2	Mwezi wa 3	Mwezi wa 4	Mwezi wa 5	Mwezi wa 6
Wiki ya 1	200.00						
Wiki ya 2	150.00						
Wiki ya 3	500.00						
Wiki ya 4	200.00						
Wiki ya 5	400.00						
Jumla ya mapato ya kila mwezi	1,450.00						

Ikiwa huna gharama za **biashara**, ruka Majedwali ya 2 na 3.

2. Pesa Zilizotumika kwa Biashara Kila Wiki

Pesa zilizotumika	Mfano	Mwezi wa 1	Mwezi wa 2	Mwezi wa 3	Mwezi wa 4	Mwezi wa 5	Mwezi wa 6
Wiki ya 1	0						
Wiki ya 2	0						
Wiki ya 3	150.00						
Wiki ya 4	0						
Wiki ya 5	30.00						
Jumla iliyotumika kila mwezi	180.00						

3. Mapato baada ya Gharama za Biashara

Ili kubainisha mapato yako baada ya gharama, ondoa **jumla ya gharama za biashara** kutoka kwa **mapato ya jumla**

	Mfano	Mwezi wa 1	Mwezi wa 2	Mwezi wa 3	Mwezi wa 4	Mwezi wa 5	Mwezi wa 6	Ongeza Mwezi wa 1 hadi Mwezi wa 6
Mapato baada ya kuondoa gharama	1,450.00 <u>- 180.00</u> 1,270.00							Jumla = _____

Ikiwa **una** gharama za biashara—

Gawanya **jumla** kwa 6. Haya ndiyo mapato yako ya wastani ya miezi 6 _____.

Ikiwa **huna** gharama za biashara—

Ongeza mwezi wa 1 hadi mwezi wa 6 kutoka kwenye visanduku vya rangi ya zambarau ilivyo katika safumlalo ya chini ya Jedwali la 1.

Jumla ya mapato ya kila mwezi								Jumla = _____
--------------------------------------	--	--	--	--	--	--	--	-------------------------

Gawanya **jumla** kwa 6. Haya ndiyo mapato yako ya wastani ya miezi 6 _____.